JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA (TBS)

MKATABA WA HUDUMA KWA WATEJA

2024

MKATABA WA HUDUMA KWA WATEJA

TBS/CSC/TOLEO NA. 3

NOVEMBA, 2024

"Shirika la Viwango Tanzania (TBS) limedhamiria, kwa kuzingatia dhamana iliyopewa, kutoa huduma bora katika utayarishaji wa viwango, usimamizi wa usalama, uhakiki wa ubora na huduma za metrolojia. TBS inahakikisha inakidhi matakwa ya kisheria, mahitaji na matarajio ya wateja, na hata kuyazidi ili kudumisha uaminifu kwao.

TBS hutoa rasilimali na kuendelea kuboresha mifumo ya utendaji wake ili kuhakikisha wakati wote wafanyakazi wake wana uwezo wa kutoa huduma bora ambazo ni endelevu."

YALIYOMO

DIBAJI.....v

1. DIRA, DHAMIRA NA MISINGI MIKUU 1

2. MADHUMUNI YA MKATABA HUU.....2

3. WATEJA WETU.....2

4. HUDUMA ZETU.....2

5. VIWANGO VYA HUDUMA ZETU.....3

6. WAJIBU WA SHIRIKA LA VIWANGO KWA WATEJA.....12

7. HAKI NA WAJIBU WA MTEJA.....13

7.1 Haki za mteja.....13

7.2 Wajibu wa mteja.....13

8. MAONI YA MTEJA KUHUSU UTOAJI WA HUDUMA.....13

9. UTAMBULISHO WA SHIRIKA NA MAELEZO YA MAWASILIANO.....14

10. UPATIKANAJI WA MKATABA.....14

CoC	Cheti Cha Ufuataji Viwango
CoR	Cheti Cha Kufaa Kuendeshwa Barabarani
GMP	Utaratibu Mzuri wa Utengenezaji
ILC	Ulinganishaji Baina ya Maabara
ISO	Shirika la Kimatiafa la Uwekaji Viwango
i-SQMT	Huduma za Uwekaji Viwango, Uhakika wa Ubora, Vipimo na Upimaji zilizounganishwa
PT	Upimaji Ubingwa
PVoC	Uhakiki wa Kabla ya Usafirishaji wa Bidhaa iwapo zimefuata viwango
TAE	Msaada wa Kiufundi kwa Wauzaji Bidhaa Nje
TBS	Shirika la Viwango Tanzania
TPC	Cheti Cha Bidhaa iliyopimwa
TT	Upimaji wa Aina ya Kitu

DIBAJI

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ni taasisi ya viwango ya umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Viwango sura ya 130. Shirika hili lilianzishwa na Serikali ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuimarisha miundombinu itakayosaidia sekta za Viwanda na Biashara kwenye uchumi nchini. Shirika hili limepewa jukumu la kutayarisha viwango, kuhamasisha uwekaji wa viwango na kuchukua hatua kwa usalama na udhibiti wa bidhaa za aina zote katika Viwanda na Biashara.

Mkataba huu wa Huduma kwa Wateja ni sehemu ya juhudi endelevu za Shirika za kuhakikisha utoaji wa huduma kwa wateja wake ni wa viwango thabiti na vya ubora wa juu, pamoja na kuhakikisha kuwa huduma hizo zinaboreshwa mara kwa mara na kufuatiliwa ipasavyo. Kupitia mkataba huu, Shirika linaweka bayana viwango na ahadi za huduma ili kutekeleza dira na dhamira yake, sambamba na mwelekeo na ari ya Serikali katika kutoa huduma bora kwa umma.

Mkataba huu wa Huduma kwa Wateja ni Toleo la Kwanza la mapitio ya Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa mwaka 2020. Mkataba huu umehuishwa ili kujumuisha mabadiliko yaliyofanywa katika Muundo wa Shirika mwaka 2021; Mpango Mkakati wa TBS (2021/2022 – 2025/2026); Utoaji wa huduma za kupima mafuta na kuzingatia miongozo mingine ya Serikali. Mkataba huu utaendelea kuhuishwa kwa kuzingatia mazingira ya utendaji kazi.

Mkataba huu unaelezea viwango vya utoaji wa huduma mbalimbali ndani ya Shirika kwa lengo la kuboresha huduma ndani na nje ya nchi ili kukidhi na kuzidi matarajio ya wateja. Aidha, unatoa maelezo ya jumla kuhusu huduma za shirika zikiwemo kazi zake kuu zinazohusu Huduma kwa Wateja, Haki za Wateja kuhusu huduma na taratibu za kushughulikia malalamiko na kupata maoni kutoka kwa wateja kuhusu ubora wa huduma zinazotolewa.

Shirika linatarajia kupata ushirikiano kutoka kwa wateja wake wote kwa kutoa maoni kuhusu huduma zinazotolewa ili kuliwezesha kuziboresha zaidi.

....

Dkt. Ashura A. Katunzi

MKURUGENZI MKUU

1.1. Dira

"Uwekaji viwango endelevu kwa maisha na ustawi wa hali ya juu wa jamii".

1.2. Dhamira

"Kuhimiza uwekaji viwango/ usalama na uhakika wa ubora katika viwanda na biashara kwa uendelezaji wa viwango, uthibitishaji, usajili, ukaguzi, upimaji na vipimo kwa maendeleo endelevu ya uchumi jamii".

1.3. Misingi yetu mikuu

Katika kuwapa huduma wateja wetu, tunaongozwa na maadili ya msingi ifuatayo:-

1.3.1. Uadilifu

Tunahakikisha tunatoa huduma bora wakati wote kwa uaminifu, bila upendeleo na kwa kuzingatia maadili ya kazi bila upendeleo kwa kufuata misingi ya maadili na unyoofu.

1.3.2. Mteja kwanza

Tunathamini wateja wetu kwa kuwapa kipaumbele katika kuwahudumia kwa wakati ili kukidhi matarajio yao.

1.3.3. Kufanya kazi kwa Ushirikiano

Tunafanya kazi kwa ushirikiano kwa kubadilishana uzoefu na kuheshimiana kufikia malengo ya taasisi.

1.3.4. Uwajibikaji

Tunawajibika katika matendo, maamuzi na matokeo ya utendaji wetu wa kazi.

1.3.5. Uwazi

Tunahakikisha tunatoa taarifa zetu kwa uwazi na kutoa mrejesho na bila upendeleo.

2. MADHUMUNI YA MKATABA HUU

Madhumuni ya Mkataba huu wa Huduma kwa Wateja ni kuwaarifu Wateja wetu, Wadau na Wananchi kwa ujumla kuhusu huduma tunazotoa na muda ambao huduma hizo zitatolewa. Aidha, Mkataba huu unaeleza haki na wajibu wa wateja wetu na njia za mawasiliano zitakazotumika, pamoja na taratibu za utoaji maoni na ushughulikiaji wa malalamiko ya wateja.

3. WATEJA WETU

Wateja wetu ni:-

i. Wizara za Serikali, Idara na Wakala;
ii. Viwanda;
iii. Wajasiriamali;
iv. Wasafirishaji na Waagizaji wa Bidhaa nje ya nchi;
v. Wananchi kwa ujumla;
vi. Kampuni zinazouza mafuta;
vii. Wabia wa maendeleo;
viii. Taasisi za Elimu na Watafiti;
ix. Hospitali;
x. Makandarasi; na
xi. Maabara.

4. HUDUMA ZETU

Shirika linatoa huduma zifuatazo: -

i. Uwekaji viwango;
ii. Mafunzo na Ushauri elekezi;
iii. Upimaji wa Bidhaa;
iv. Ugezi;
v. Upimaji Ubingwa au Ulinganishaji baina ya Maabara;
vi. Uthibitisho;
vii. Usajili;
viii. Ripoti/ Taarifa zinazohusiana na Shirika;

ix. Kuondoa bidhaa zisizofaa/hafifu,bandia au zilizopigwa marufuku;
x. Ukaguzi wa bidhaa zilizoingizwa nchini;
xi. Upimaji wa Mafuta;
xii. Huduma nyingine.

5. VIWANGO VYA HUDUMA ZETU

Tunatoa Huduma kwa Wateja wetu kwa kuzingatia viwango vifuatavyo:

5.1 Uwekaji wa Viwango

Na	Huduma	Viwango vya Huduma
5.1.1	Utoaji wa waraka wa viwango vilivyopo	Ndani ya saa (3) za kazi baada mteja kutimiza vigezo vilivyowekwa
5.1.2	Utayarishaji wa waraka mpya wa viwango	Ndani ya mwaka mmoja
5.1.3	Utoaji wa tafsiri ya kiufundi na maelezo kuhusu kiwango na uainisho au vipimo kamili	Ndani ya siku tano (5) za kazi

5.2 Mafunzo na Ushauri Elekezi

Na	Huduma	Viwango vya Huduma
5.2.1	Utoaji wa mafunzo kuhusu uwekaji viwango, udhibiti ubora, uhakika wa ubora na mbinu za maabara na utoaji wa cheti	Ndani ya siku (7) za kazi baada ya kumaliza mafunzo

5.2.2	Utoaji wa huduma za ushauri elekezi kuhusu viwango, uhakiki wa ubora, usalama, vipimo na utoaji wa ripoti	Ndani ya siku tano (5) za kazi baada ya kumaliza ushauri elekezi

5.3 Upimaji wa Bidhaa

Na	Huduma	Viwango vya Huduma
5.3.1	Utoaji wa ripoti ya vifaa au nyenzo za ujenzi, ufundi mitambo/makanika na umeme kwa ombi la mteja/upimaji wa aina ya kitu (TT)	Ndani ya siku tano (5) za kazi baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa
5.3.2	Utoaji wa ripoti ya upimaji kwa bidhaa za mabomba, sola na betri	Ndani ya siku kumi (10) za kazi baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa
5.3.3	Utoaji wa ripoti ya upimaji kwa bidhaa za saruji na bidhaa zinazohusiana na saruji	Ndani ya siku 35 za kazi baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa
5.3.4	Utoaji wa ripoti ya upimaji kwa bidhaa za kemia ya chakula/ sampuli kwa ombi la mteja/upimaji wa aina ya kitu (TT)	Ndani ya siku kumi (10) za kazi baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa

Na	Huduma	Viwango vya Huduma
5.3.5	Utoaji wa ripoti ya upimaji kwa sampuli za mikrobiolojia kwa ombi la mteja/upimaji wa aina ya kitu (TT)	Ndani ya siku kumi (10) za kazi baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa
5.3.6	Utoaji wa ripoti ya upimaji kwa sampuli za bidhaa za kikemikali na mazingira kwa ombi la mteja/upimaji wa aina ya kitu (TT)	Ndani ya siku kumi (10) za kazi baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa
5.3.7	Utoaji wa ripoti ya upimaji kwa vifungashio na nyenzo za vifungashio kwa ombi la mteja/ upimaji wa aina ya kitu (TT)	Ndani ya siku tano (5) za kazi baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa
5.3.8	Utoaji wa ripoti ya upimaji wa bidhaa za vitambaa na ngozi kwa ombi la mteja/ upimaji wa aina ya kitu (TT)	Ndani ya siku saba (7) za kazi baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa

5.4 Ugezi

Na	Huduma	Viwango vya Huduma
5.4.1	Utoaji wa cheti cha ugezi, kwa vifaa, geji na zana za kisayansi za kupima umakini mahali pa mradi	Ndani ya siku 20 za kazi baada ya uthibitisho
5.4.2	Utoaji wa cheti cha ugezi kwa vifaa, na zana za kisayansi za kupima umakini	Ndani ya siku 10 za kazi baada ya kuwasilisha zana

5.4.3	Utoaji wa msaada wa kiufundi kwa masuala ya vipimo (Metrology) na utoaji wa ripoti	Ndan ya siku saba (7) za kazi baada ya kumalizika msaada wa kiufundi
5.4.4	Utoaji wa kibali cha kushuhudia ugezi	Ndani ya siku mbili (2) za kazi

5.5 Upimaji Ubingwa au Ulinganishaji Baina ya Maabara

Na	Huduma	Viwango vya Huduma
5.5.1	Utoaji taarifa kwa maabara kuhusu nia ya utaoji wa upimaji ubingwa au ulinganishaji sampuli baina ya maabara	Siku 90 kabla ya kuanza PT/ILC
5.5.2	Utoaji taarifa kwa maabara zinazofanyiwa tathimini ya umahiri	Ndani ya siku 30 kabla ya usambazaji wa sampuli za PT/ ILC
5.5.3	Utoaji wa matokeo ya PT/ILC	Ndani ya siku 45 baada ya usambazaji wa sampuli
5.5.4	Utoaji wa ripoti ya tathmini ya PT/ILC	Ndani ya siku 35 baada ya kupokea matokeo kutoka maabara iliyofanyiwa tathimini ya umahiri

5.6 Utoaji wa Leseni

Na	Huduma	Viwango vya Huduma
5.6.1	Utoaji wa waraka wa viwango vilivyopo	Ndani ya saa tatu (3) za kazi baada mteja kutimiza vigezo vilivyowekwa

5.6.2	Saruji na bidhaa zinazohusiana na saruji	Ndani ya siku 27 za kazi baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa
5.6.3	Utoaji wa idhini ya kuongeza muda wa leseni kutumia alama ya viwango/ TPC	Ndani ya siku 45 baada ya usambazaji wa sampuli
5.6.4	Utoaji wa leseni ya kutumia alama ya viwango/ TPC kwa viwanda vilivyopo nje ya nchi	Ndani ya siku 30 baada ya ukaguzi
5.6.5	Utoaji wa cheti cha mfumo wa usimamizi	Ndani ya miezi sita (6) baada ya ukaguzi wa hatua ya kwanza kwa viwango vya mfumo wa usimamizi, kulingana na kutimizwa kwa masharti yanayotakiwa. Mfumo wa usimamizi unajumuisha yafuatayo:-
		• ISO 9001: Mfumo wa Usimamizi wa Ubora (QMS);
		• ISO 22000: Mfumo wa Usimamizi wa Uhakika wa Chakula (FSMS);
		•TZS 1770: Uchambuzi wa vihatarishi na maeneo muhimu ya Kudhibiti (HACCP);
		•ISO 21001: Mfumo wa Usimamizi wa Uendeshaji wa Elimu (EOMS);

		• ISO 14001: Mifumo ya Usimamizi wa Mazingira(EMS);
		• ISO 45001:Mifumo ya Usimamizi wa Usalama na Afya mahali pa kazi (OH & SMS); na
		•ISO 50001: Mfumo wa Usimamizi wa Nishati (EnMS).

5.7 Usajili

Na	Huduma	Viwango vya Huduma
5.7.1	Usajili wa majengo na utoaji wa vibali vya usajili wa majengo yasiyo ya utengenezaji kwa ajiili ya chakula na vipodozi	Ndani ya siku saba (7) za kazi baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa
5.7.2	Utoaji wa kibali cha uongezaji muda wa usajili wa majengo kwa majengo yasiyo ya utengenezaji kwa ajili ya chakula na vipodozi	Ndani ya siku mbili (2) za kazi baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa

5.7.3	Usajili na utoaji wa cheti cha kuongeza muda wa usajili wa vyakula na vipodozi vilivyoingizwa nchini vikiwa vimefungashwa	Ndani ya siku 24 za kazi baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa
5.7.4	Utoaji wa cheti cha kuongeza muda wa usajili wa vyakula na vipodozi vilivyoingizwa nchini vikiwa vimefungashwa	Ndani ya siku 24 za kazi
5.7.5	Utoaji wa Cheti cha Utaratibu Mzuri wa Utengenezaji (GMP) kwa bidhaa za vyakula hatarishi zaidi	Ndani ya siku 30 baada ya kukamilisha ukaguzi wa GMP
5.7.6	Utoaji wa idhini ya vifaa vya matangazo na uhamasishaji wa bidhaa za vyakula na vipodozi	Ndani ya siku 10 za kazi baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa
5.7.7	Utoaji wa ripoti ya tathmini ya usanifu wa lebo	Ndani ya siku saba (7) za kazi

5.8 Ripoti/Taarifa zinazohusiana na Shirika

Na	Huduma	Viwango vya Huduma
5.8.1	Utoaji wa taarifa kuhusu kviwango, uhakika wa ubora, vipimo,usalama na mambo ya upimaji	Ndani ya siku mbili (2) za kazi baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa
5.8.2	Utoaji wa ripoti kuhusu msaada wa kiufundi kwa wasafirishaji wa bidhaa za nje (TAE) kwa bidhaa za zilizo thibitishwa na vifurushi vidogo vya chini ya kilo	Ndani ya siku moja (1) ya kazi baada ya kutimiza mahitaji
5.8.3	Utoaji wa ripoti kuhusu msaada wa kiufundi kwa wasafirishaji bidhaa za nje (TAE) kwa bidhaa zisizo thibitishwa	Ndani ya siku (10) za kazi baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa

5.9 Kuondoa bidhaa zisizofaa, hafifu, bandia au zilizopigwa marufuku

Na	Huduma	Viwango vya Huduma
5.9.1	Utoaji wa cheti cha uondoaji wa bidhaa zisizofaa, hafifu, bandia au zilizo pigwa marufuku	Ndani ya siku mbili (2) za kazi baada ya kumaliza uondoaji

5.10 Ukaguzi wa bidhaa zilizoingizwa nchini

Na	Huduma	Viwango vya Huduma
5.10.1	Utoaji wa cheti cha bechi kwa bidhaa za kawaida zilizoingizwa nchini	Ndani ya saa 48 baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa
5.10.2	Utoaji wa kibali cha bidhaa zilizoingizwa nchini kwa bidhaa za kawaida na shehena nyevu	Ndani ya siku mbili (2) baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa
5.10.3	Utoaji wa notisi ya kuruhusu shehena nyevu	Ndani ya saa sita (6) baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa
5.10.4	Utoaji wa cheti cha kufaa kuendeshwa barabarani (CoR) kwa magari yaliyotumika yaliyoingizwa nchini	Ndani ya siku moja (1) baada ya ukaguzi
5.10.5	Utoaji wa cheti cha ufuataji viwango (CoC) kwa bidhaa za kawaida zilizoingizwa nchini	Ndani ya saa 48 baada ya kupokea ombi

5.11 Upimaji wa Mafuta

Na	Huduma	Viwango vya Huduma
5.11.1	Alama ya bidhaa za petroli	Dakika 30 baada ya kutimiza vigezo vilivyowekwa

5.12 Huduma nyingine

Na	Huduma	Viwango vyaHuduma
5.12.1	Kujibu malalamiko ya mteja	Ndani ya siku 14 za kazi baada ya kusajili kwa malalamiko yasiyo ya uchunguzi na muhimu
5.12.2	Kujibu malalamiko ya mteja	Ndani ya siku 30 baada ya kusajili kwa malalamiko ya uchunguzi
5.12.3	Kujibu hoja za mteja	Ndani ya siku moja (1) ya kazi
5.12.4	Kujibu simu zote zinazopigwa ndani	Miito mitatu (3)
5.12.5	Kujibu barua/ baruapepe za mteja	Ndani ya siku tano (5) za kazi baada ya kupokea
5.12.6	Kukiri kupokea barua ya mteja	Ndani ya siku mbili (2) za kazi

6. WAJIBU WA SHIRIKA LA VIWANGO KWA WATEJA

Shirika litakuwa na wajibu ufuatao: -

i. Kutoa huduma kwa wakati na bila upendeleo;
ii. Kuheshimu faragha na utu wa wateja;
iii. Kuwa na msaada, ukarimu na kuwazingatia wenye mahitaji maalumu;
iv. Kutoa huduma kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zinazotawala; na
v. Kushughulikia malalamiko na hoja za wateja kwa wakati.

7. HAKI NA WAJIBU WA MTEJA

7.1 Haki ya Mteja

Mteja ana haki zifuatazo: -

i. Kupata huduma bora;

ii. Kushughulikiwa haraka kwa utu, heshima na uwazi bila upendeleo;

iii. Kutoa malalamiko au mapendekezo kwa Shirika bila kubugudhiwa;

iv. Kupata taarifa zilizohuishwa kuhusu huduma za TBS, na

v. Kuwa na faragha na usiri katika kushughulikia taarifa.

7.2 Wajibu wa Mteja

Mteja ana wajibu ufuatao: -

i. Kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zinazotawala;

ii. Kuhudhuria kwa wakati shughuli zilizopangwa na Shirika;

iii. Kuwaheshimu wafanyakazi wa TBS; na

iv. Kutoa kwa haraka na usahihi taarifa zinazotakiwa na zinazofaa kwa Shirika.

8. MAONI YA MTEJA KUHUSU UTOAJI WA HUDUMA

Wateja wana haki ya kutoa maoni kwa ukamilifu, mapendekezo na/ au malalamiko kwa TBS kupitia TBS i-SQMT Portal (www.tbs.go.tz>e-services>i-SQMT portal>complaints or enquiry), e-Mrejesho, yeye mwenyewe, kupiga simu ya bure (0800110827), kupitia baruapepe (complaints@tbs.go.tz/malalamiko@tbs.go.tz), Simu, kutuma kwenye mitandao yetu ya kijamii: Twitter (TBS_Tanzania), Instagram (tbs_viwango), YouTube (TBS Viwango TV) na masanduku ya maoni yaliyopo kwenye ofisi zote za TBS.

TBS imedhamiria kushukuru kwa haraka maoni yote ya wateja na kushughulikia malalamiko yote na mapendekezo kwa ajili ya uboreshaji wa kudumu wa utoaji huduma.

9. UTAMBULISHO WA SHIRIKA NA MAELEZO YA MAWASILIANO

Ofisi za Makao Makuu ya Shirika la Viwango Tanzania ziko jijini Dar es Salaam kwenye makutano ya barabara ya Morogoro/ Sam Nujoma, wilaya ya Ubungo. Shirika lina ofisi (9) za kanda Tanzania Bara.

10. UPATIKANAJI WA MKATABA

Baada ya uzinduzi, mkataba utapatikana kupitia Tovuti na Makta-ba ya Shirika.

MKURUGENZI MKUU

Shirika la ViwangoTanzania (TBS),
Makutano ya barabara ya Morogoro/
Sam Nujoma, Ubungo
S.L.P 9524 Dar es Salaam, Tanzania.
Simu:+255 22 2450206
Baruapepe:info@tbs.go.tz
Tovuti:www.tbs.go.tz
Namba ya simu ya bure: 0800110827

OFISI YA UDHIBITI WA BIDHAA ZIINGIAZO NA ZITOKAZO NCHINI

TPA One Stop Centre Bandari House,
Ghorofa ya 8 barabara ya Sokoine
Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 737 776 721
+255 737 776 718
+255 738 045 157

OFISI ZA KANDA

KANDA YA DAR ES SALAAM

(Ilala, Temeke, Kigamboni, Kinondoni na Ubungo)
Jengo la PSSSF Commercial Complex Ghorofa ya 4 Sam Nujoma Road
S.L.P 9525 Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: 0738 746326

Ofisi ya Mbweni
Simu: +255 735006976

KANDA YA MASHARIKI

(Pwani, Tanga na Morogoro)
Halmashauri ya Mji wa Kibaha
Kibaha

Ofisi ya Bagamoyo
Simu: +255 738045170
Bandari ya Tanga
Simu: +255 767276861

OFISI ZA MIPAKANI KANDA YA MASHARIKI

Mpaka wa Horohoro
Simu: +255 756554667

KANDA YA KATI

(Dodoma, Iringa na Singida)
Jengo la PSSSF Kambarage Tower
Ghorofa ya 6
S.L.P 2956 Dodoma, Tanzania
Simu: +255 0262963865
+255 768352006

KANDA YA KASKAZINI

(Arusha, Kilimanjaro na Manyara)
Ngorongoro Tourism Centre Building
Ghorofa ya 6 Mtaa wa Goriondoi
S.L.P 2399 Arusha, Tanzania.
Simu: +255 0272520143
+255 0766120418

OFISI ZA MIPAKANI KANDA YA KASKAZINI

Uwanja wa ndege Kilimanjaro (KIA)
Simu: +255 753965567
Mpaka wa Namanga
Simu: +255 768387409
Mpaka wa Tarakea
Simu: +255 0766102697
Mpaka wa Holili
Simu: +255 745446567

KANDA YA ZIWA MAGHARIBI
(Geita, Kagera na Shinyanga)
Ofisi ya Kamishna wa Mkoa
S.L.P 816
Magongo – Geita

OFISI ZA MIPAKANI KANDA YA ZIWA MAGHARIBI
Mpaka wa Mutukula
Simu: +255 768377574
Mpaka wa Kabanga
Simu: +255 746 435439

Mpaka wa Rusumo
Simu: +255 769423142
Simu: +255 0272520143
+255 0766120418

KANDA YA ZIWA MASHARIKI
(Mwanza, Simiyu na Mara)
Jengo la NSSF Ghorofa
ya 3 Barabara ya Kenyata
S.L.P 1814 Mwanza, Tanzania
Simu: +255 0282505044
+255 768342355

OFISI ZA MIPAKANI KANDA YA ZIWA MASHARIKI
Uwanja wa Ndege Mwanza
Simu: +255 745768990
Bandari ya Mwanza
Simu: +255 754839984
Mpaka wa Sirari
Simu: +255 769395368

KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI
(Mbeya, Songwe, Rukwa na Njombe)
Jengo la NHIF Ghorofa ya 7 Barabara ya Avenue
S.L.P 1674 Mbeya, Tanzania
Simu: +255 0252502848
+255 0767217268

OFISI ZA MIPAKANI KANDA YA ZIWA MASHARIKI
Mpaka wa Tunduma
Simu: +255 752046646
Mpaka wa Kasumulu
Simu: +255 766020442

KANDA YA KUSINI
(Mtwara, Lindi na Ruvuma)
Jengo la PSSSF Sokoine House
Ghorofa ya 3 Mtaa wa Raha
S.L.P 1396 Mtwara, Tanzania
Simu: +255 0232334477
+255 767247398

KANDA YA MAGHARIBI
(Kigoma, Katavi na Tabora)
Jengo la NSSF Mafao House Ghorofa ya 2 Mnarani Area Manispaa ya Kigoma Ujiji
S.L.P 1276 Kigoma, Tanzania
Simu: +255 0282804023
+255 769421603

"TUMIA BIDHAA ZILIZOTHIBITISHWA UBORA WAKE NA TBS"

"Kujenga uzoefu mzuri wa mteja hakutokei kwa bahati''

"Ili kutoa huduma ya uhakika ni lazima uongeze kitu ambacho hakiwezi kununuliwa au kupimwa kwa pesa, na kitu hicho ni uaminifu na uadilifu"

"Huduma kwa wateja sio idara, ni kazi ya kila mtu''